# Ukatili kwa Wanawake wanaoishi na HIV kutoka kwa wapenzi wao wa karibu: maswali na majibu

Machi 2016

## Utangulizi

**Je, mwongozo huu ni wa nani?**
Mwongozo huu ni wa wanawake, pamoja na wanawake waliobadilisha jinsia, ambao wanaishi na HIV na ambao wanapitia au wako katika hatari ya kupitia ukatili kutoka kwa wapenzi wao wa karibu. Ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu unaweza kuwa wa kimwili, kihisia, kisaikolojia au unyanyasaji wa kingono kutoka kwa mtu ambaye una au umekuwa na mahusiano ya karibu naye. Dhuluma kutoka kwa mpenzi wa karibu sio mbaya tu - bali ni kinyume cha sheria. Ilhali, ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu ni mojawapo ya aina za ukatili zinazojulikana sana dhidi ya wanawake.

**Mwongozo huu unakupa maelezo ya kisheria, sio ushauri wa kisheria**
Mwongozo huu unakupa maelezo kuhusu sheria tofauti ambazo zinaweza kutumika kwa wanawake wanaopitia ukatili kutoka kwa wapenzi wa karibu, ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu jinsi sheria ya jinai inavyoathiri mahusiano ya karibu kwa watu wanaoishi na HIV. Mwongozo huu unalenga sheria ambazo zinatumika Ontario, lakini baadhi ya sehemu (kwa mfano, sehemu ya sheria ya jinai) inatumika pia katika mikoa na himaya yote nchini Canada. Mwongozo huu hautoi ushauri wa kisheria kuhusu hali yako maalum. Ikiwa unataka au unahitaji ushauri wa kisheria, unapaswa kuongea na wakili. Ikiwa unaishi na HIV, unaweza kuwasiliana na Kliniki ya Kisheria ya HIV na Ukimwi iliyoko Ontario (HALCO). Kuna maelezo mwishoni mwa mwongozo huu kuhusu ni wapi unaweza kupata msaada.

**Je, ni kwa nini kuna mwongozo kuhusu ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu kwa wanawake wanaoishi na HIV?**
Ijapokuwa ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu unaweza kufanyika katika mahusiano kati ya watu wa jinsia zote, tunalenga masuala ambayo yanawaathiri wanawake wanaoishi na HIV kwa sababu watu wengi wanaoathiriwa na ukatili kutoka kwa wapenzi wa karibu ni wanawake. Kwa kawaida huwa ni wanaume (waume, wanandoa, wapenzi wa kisheria au marafiki wa kiume) wanaotekeleza dhuluma hii, lakini sheria hizi zinatumika pia kwa wanyanyasaji wa jinsia moja.

Huenda mwanamke akaogopa kumweleza mpenzi wake kwamba ana HIV kwa sababu anaogopa mpenzi wake atakuwa mkatili. Huenda akaogopa kupata matibabu kwa sababu anaogopa dhuluma. Ukatili unaweza pia kuanza au kukithiri wakati wa ujauzito na huu unaweza kumzuia mwanamke kutafuta matibabu ya kuzuia maambukizi ya HIV kwa mtoto wakati wa ujauzito na kujifungua.

Sheria inaweza kuwa ngumu sana. Wanawake wanaoishi na HIV ambao wanapitia ukatili kutoka kwa wapenzi wao wa karibu wanaweza kukabiliana na matatizo magumu ya kisheria. Mfumo wa kisheria ni mgumu zaidi kwa wanawake ikiwa ni kina mama, walemavu, wamebaguliwa kiumbari, wenyeji, wageni nchini Canada au si raia wa Canada. Wanawake wanaoishi na HIV huenda wakawa na wasiwasi kuhusu faragha na ufichuzi wa hali yao ya HIV. Mwongozo huu unasaidia kuwafahamisha wanawake wanaoishi na HIV kuhusu sheria muhimu za jinai, faragha, familia, uhamiaji na afya ya umma, na jinsi HIV inavyoweza kuathiri jinsi ambavyo sheria zinaweza kutumika.

Mfumo wetu wa kisheria bado haujashughulikia masuala tata yanayohusiana na HIV na ukatili kutoka kwa wapenzi wa karibu. Hali na mahitaji ya kila mwanamke ni tofauti na maelezo ya kisheria hayashughulikii kila hali. Baadhi ya wanawake wanaweza kuamua kutoenda kwa polisi au mahakamani. Mwongozo huu umebuniwa kukupa baadhi ya maelezo muhimu kuhusu haki zako na mfumo wetu wa kisheria ili kukusaidia kufanya maamuzi bora kwa ajili yako mwenyewe.

Hakuna mtu anayestahili kupitia ukatili au dhuluma na iwapo unapitia ukatili kutoka kwa mpenzi wako wa karibu, hustahili kujilaumu. Kuna hatua unazoweza kuchukua ili kujilinda vyema pamoja na watoto wako dhidi ya dhuluma katika uhusiano wa karibu, na kuna huduma ambazo zinaweza kukusaidia. Wakili anaweza kukupa ushauri wa kisheria kuhusu machaguo yako. Unaweza pia kuamua kuongea na mshauri nasaha katika kituo cha unyanyasaji wa kingono, makao ya wanawake au shirika la huduma za UKIMWI (ASO). Huenda mshauri nasaha akaweza kukupa msaada na usaidizi. Kuna viungo vya baadhi ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu.

## Machaguo ya kisheria kwa wanawake wanaoishi na HIV ambao wanapitia ukatili kutoka kwa wapenzi wao wa karibu

**Je, ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu ni hatia nchini Canada?**
Baadhi ya tabia za dhuluma (kama vile vitendo na maneno) zinazingatiwa kuwa uhalifu. Hizi ni pamoja na:

- kutumia nguvu au kumdhuru mtu kimwili, hata kama hakuna majeraha (shambulizi);
- kumlazimisha mtu kufanya vitendo vya ngono (unyanyasaji wa kingono);
- kumtisha mtu na madhara au ngono asiyotaka, au kujaribu kumshambulia au kumnyanyasa mtu kingono;
- kumnyanyasa au kumnyemelea mtu (unyanyasaji wa jinai); na
- kutumia nguvu kumpeleka au kumweka mtu pahali fulani, bila mamlaka ya kisheria (kumzuia mtu kwa nguvu).

Mashtaka ya jinai yanaweza kujumuisha, shambulizi, unyanyasaji wa kingono, kutoa vitisho, unyanyasaji wa jinai na kumzuia mtu kwa nguvu. Mashtaka ya unyanyasaji wa kingono yanaweza kufunguliwa iwapo mtu, ikiwa ni pamoja na mwanamke mwenye HIV, hajafichua hali

yake ya HIV kabla ya tendo la ngono wakati kuna “uwezekano wa kweli” wa maambukizi ya HIV (angalia sehemu iliyoko hapa chini yenye mada “Sheria ya jinai na HIV”).

**Unawezaje kuripoti jinai?**
Ikiwa ni hali ya dharura kwa sababu wewe au mtu mwingine ako hatarini, unaweza kupiga simu kwa 911, ambayo ni nambari ya dharura nchini Canada. Mhudumu wa huduma za dharura ataongea na wewe na anaweza kuwatuma polisi au msaada mwingine wa dharura, kama vile ambulensi. Iwapo unahitaji mkalimani, mhudumu wa 911 anaweza kumpata mkalimani kupitia simu. Iwapo umejeruhiwa, unapaswa kupata matibabu.

Unapaswa kusoma kijitabu hiki ili ujifunze kuhusu mambo unayopaswa kuyazingatia kabla ya kuamua kupiga simu au kuwatembelea polisi. Ni wazo nzuri kupata ushauri wa kisheria kutoka kwa wakili wa jinai na kutoka kwa wakili wa uhamiaji (ikiwa wewe si raia wa Canada) kabla ya kwenda kwa polisi au kuchukua hatua nyingine chini ya sheria ya jinai. Ukiamua kuripoti ukatili kwa polisi, watachunguza malalamiko yako na kuamua kama kuna maelezo ya kutosha kwamba kosa lilitokea ili kufungua mashtaka ya jinai. Polisi wataweka muhtasari wa uchunguzi huo.

Inaweza kuwa vigumu kukumbuka maelezo baadaye kwa hivyo ni muhimu uandike muhtasari wa yaliyotendeka.  Andika tarehe, saa, eneo na majina ya kila mtu aliyekuwa hapo. Weka maelezo hayo katika mahali salama. Ni muhimu pia kujua kwamba ikiwa utaongea na wataalamu wengine kuhusu dhuluma hiyo (kwa mfano, daktari, mhudumu wa jamii au mshauri nasaha), kuna uwezekano kwamba wataweka muhtasari kuhusu ulichoripoti. Fahamu pia kwamba wakati unaongea na mtu mwingine kuhusu dhuluma hiyo, iwe mtaalamu au la (kwa mfano, rafiki, jamaa, jirani au mfanyakazi mwenza), maelezo haya yanaweza kutumika katika kesi ya mahakamani. Katika hali nyingine, maelezo haya yanaweza kutumika dhidi yako, hata kama wewe ndiye mlalamishi wa dhuluma. Kwa mfano, inaweza kusemekana kwamba mahakama haipaswi kukuamini iwapo uliwaeleza watu mambo tofauti kuhusu kilichofanyika.

**Itakuwaje iwapo polisi hawatamshtaki aliyekunyanyasa?**
Ikiwa polisi hawatamshtaki aliyekunyanyasa, unaweza kufungua mashtaka wewe mwenyewe. Utalazimika kwenda mahakamani na “kuwasilisha taarifa binafsi.” Utamwomba Jaji wa Amani wa mahakama kufungua mashtaka dhidi ya mtu huyo, kulingana na utakachomwelezea Jaji huyo wa Amani kuhusu hali hiyo. Utalazimika kuelezea kweli kwa kuandika na kuahidi kwamba unachosema ni kweli. Jaji wa Amani ataamua kama kuna maelezo ya kutosha kwamba kosa lilifanyika ili kufungua mashtaka ya jinai. Mchakato huu unaweza kuwa mgumu, kwa hivyo ni vyema kama unaweza kupata ushauri wa wakili kabla ya kwenda mahakamani.

**Je, ni nini hufanyika iwapo aliyekunyanyasa ameshtakiwa?**
Iwapo mashtaka yatafunguliwa na polisi au Jaji wa Amani, wakili wa serikali (“Mwendesha mashtaka”) atachukua kesi hiyo ya mahakama ya jinai dhidi ya mnyanyasaji. Mwendesha mashtaka si wakili wako na anaweza kuendelea na kesi hiyo hata kama utaamua kwamba hutaki kuendelea na kesi hiyo. Huna haki ya kukomesha kesi ya jinai. Kuna uwezekano kwamba utakuwa shahidi katika kesi hiyo ya mahakama na unaweza kulazimika kwenda mahakamani.

**Je, utalazimika kuwaeleza polisi kuwa una HIV?**
Kwa kawaida huhitajiki kisheria kutoa maelezo kuhusu hali yako ya HIV kwa polisi. Hata hivyo, polisi wanaweza kujua hali yako wakati wa uchunguzi wao.

**Je, hali yako ya HIV inaweza kufichuliwa ukiripoti uhalifu?**

Ikiwa polisi watamshtaki aliyekunyanyasa, huenda wakili wakajua kuhusu hali yako ya HIV kutoka kwa taarifa yako kwa polisi, kwa kuomba mahakamaruhusa ya kupata rekodi zako za matibabu, au kwa sababu ya unachosema mahakamani. Ukiwasilisha taarifa binafsi kwa Jaji wa Amani, hali yako ya HIV inaweza kutokea wakati unaelezea hadithi yako kwa mahakama. Huenda pia hali yako ya HIV ikatokea katika uamuzi wa mahakama, ambao kwa kawaida hupatikana kwa umma na unaweza kufika kwa vyombo vya habari. Iwapo hali yako ya HIV imejumuishwa katika uamuzi wa mahakama, polisi, mamlaka ya uhamiaji na mwananchi yeyote anaweza kujua kuhusu hali yako ya HIV, ambayo inaweza kutumika dhidi yako kwa njia ambazo hutarajii. Unaweza kuomba mahakama kuamua kama itaficha jina lako na maelezo mengine ambayo yanaweza kutambua utambulisho wako, kwa mfano, kutumia herufi za kwanza za majina yako au kupiga marufuku mtu yeyote dhidi ya kushiriki jina lako hadharani. Ikiwa una HIV, unapaswa kupata ushauri kutoka kwa wakili wa jinai kuhusu kulinda faragha yako kabla ya kuripoti dhuluma.

**Itakuwaje kama ninaripoti uhalifu unaohusiana na HIV?**
Katika hali nyingine, mtu anaweza kushtakiwa kwa uhalifu iwapo anajua ana HIV na afanye mapenzi bila kumweleza mpenzi wake kuhusu hali yake ya HIV (imefafanuliwa kikamilifu hapa chini katika sehemu yenye mada “Sheria ya jinai na HIV”). Ukimripoti aliyekunyanyasa kwa kutokueleza hali yake ya HIV kabla ya kufanya mapenzi, polisi watakuuliza kama umepatikana kuwa una HIV. Ukikataa kujibu, polisi, Mwendesha mashtaka au wakili wa utetezi wanaweza kuomba mahakama kutoa amri ya kupata rekodi zako za matibabu au rekodi nyingine zenye maelezo kuhusu hali yako ya HIV. Tafadhali wasiliana na HALCO au wakili mwingine kabla ya kwenda kwa polisi iwapo unafikiria kumripoti aliyekunyanyasa kwa kutofichua hali yake ya HIV.

**Je, ni nini hufanyika baada ya kuripoti mpenzi wako kwa sababu ya unyanyasaji?**
Unaporipoti ukatili kutoka kwa mpenzi wako wa karibu kwa polisi, watakuuliza maelezo ya ndani kuhusu dhuluma hiyo. Polisi pia watapata maelezo kwa kuongea na aliyekunyanyasa na ikiwezekana wanafamilia, majirani au watu wengine wanaoweza kujua jambo lolote kuhusu hali yako au uhusiano wenu.

Iwapo polisi watapata kuwa mpenzi wako wa karibu alikushambulia, ni lazima wafungue mashtaka. Hii inaitwa “sera ya lazima ya kufungua mashtaka.” Iwapo polisi watapata kwamba nyinyi wote mlihusika katika vitendo vya fujo, watalazimika kujaribu kubainisha ni nani aliyeanzisha mzozo huo, au ni mhusika gani mkuu katika vitendo vya ukatili. Wakati mwingine wahusika wote hushtakiwa.

Katika hali hizi, huenda mnyanyasaji akajaribu kukushtaki kwa kutekeleza uhalifu. Kwa mfano, anaweza kusema wewe ndiwe uliyemshambulia, na kama una HIV, anaweza kudai kwamba hukumwambia kwamba una HIV kabla ya kufanya mapenzi naye mara ya kwanza (angalia sehemu hapa chini inayohusu, “Sheria ya jinai na HIV”). Ikiwa uko hatarini, usalama wako ndio jambo muhimu kabisa, na huenda ukahitaji kwenda kwa polisi. Ikiwa una wasiwasi kwamba mpenzi wako atakushtaki kwa kuwa na HIV na kutomwambia kabla ya kufanya mapenzi, unapaswa kuongea na wakili wa jinai kabla ya kwenda kwa polisi. Ukishtakiwa, ni muhimu kwamba uongee na wakili wa jinai haraka iwezekanavyo.

Ukiripoti ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu na mashtaka yafunguliwe dhidi ya aliyekunyanyasa, Mwendesha mashtaka atakuuliza maswali. Huenda pia ukaombwa uende Mahakamani kuelezea kilichokufanyikia (inaitwa “kutoa ushahidi”). Wakati inashughulikia mashtaka ya unyanyasaji wa kingono, kwa kawaida mahakama haitaruhusu maswali kuhusu historia yako ya kingono, lakini huenda ukaulizwa maswali kadha wa kadha. Ikiwa unamshtaki

aliyekunyanyasa kwa kutofichua hali yake ya HIV, mahakama inaweza kuruhusu maswali zaidi kuhusu historia yako ya kingono.

Wizara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina mpango ambao unawasaidia walalamikaji wa ukatili na unyanyasaji wa kingono kutoka kwa wapenzi wa karibu, unaoitwa Mpango wa Kuwasaidia Waathirika (Victim Witness Assistance Programu -VWAP). VWAP hutoa msaada wa kihisia na rufaa kwa huduma za ushauri kwa waathirika wa uhalifu, na hata pia maelezo kuhusu mfumo wa mahakama ya jinai. Wahudumu wa VWAP hukusaidia kijiandaa kwa ajili ya mahakama na hukusaidia kuwasiliana na Mwendesha mashtaka. Vituo vya unyanyasaji wa kingono vinaweza pia kukupa maelezo na usaidizi. Ikiwa unamuogopa mpenzi wako, unaweza kuwasiliana na VWAP au kituo cha unyanyasaji wa kingono. Unapaswa kupiga simu kwa HALCO kwa ushauri wa kisheria iwapo una wasiwasi kuhusu hali yako ya HIV kufichuliwa au ikiwa una wasiwasi kuhusu kushtakiwa kwa kutofichua hali yako ya HIV. Angalia sehemu ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu ili upate maelezo ya mawasiliano ya VWAP, vituo vya unyanyasaji wa kingono na HALCO.

**Je, unaweza kufanya nini ili kujiweka salama?**
**Ikiwa aliyekunyanyasa ameshtakiwa:** Anaweza kukamatwa na kuachiliwa, au anaweza kuwekwa korokoroni kwa muda, au hadi kesi ikamilike. Iwapo una wasiwasi kwamba akiachiliwa atakunyanyasa, kukutisha au kukudhuru, waeleze polisi. Anaweza kuwekwa jelani hadi wakati wa kusikilizwa kwa kesi mahakamani, au anaweza kuachiliwa kwa masharti yanayosema kwamba haruhusiwi kuwasiliana na wewe kwa njia yoyote ile na kwamba hawezi kukukaribia. Wakati kesi imeanza kupitia mchakato wa mahakama, VWAP itawasiliana na wewe kukufafanulia ni nini kitakachofuata. Ikiwa bado unaogopa kwamba mpenzi wako anaweza kuwasiliana na wewe au kukudhuru, mweleze mhudumu wa VWAP au Mwendesha mashtaka.

Ikiwa aliyekunyanyasa anatumia hali yako ya HIV kukuumiza (kwa mfano, anawaelezea watu kuhusu hali yako ya HIV, au anakuzuia kupata dawa au matibabu yako), unapaswa kumweleza mhudumu wako wa VWAP au Mwendesha mashtaka, na ufikirie kuongea na wakili kuhusu mambo mengine unayoweza kufanya ili kujilinda.

Unaweza kuwasiliana na Mpango wa Usaidizi wa Kisheria wa Ontario wa Kukomesha Ukatili dhidi ya Familia - Legal Aid Ontario Family Violence Authorization Program ili kuona kama unafaa kupokea saa mbili za ushauri wa kisheria bila malipo unaohusiana na ukatili unaotoka kwa mpenzi wa karibu. Maelezo yanapatikana kwa zaidi ya lugha 200. Angalia sehemu ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu kwa maelezo ya mawasiliano.

**Iwe aliyekunyanyasa ameshtakiwa au la:** Ikiwa unaogopa kwamba aliyekunyanyasa anaweza kukuumiza, unaweza kuomba amri ya mahakama ili kukusaidia kukulinda. Ikiwa uliishi na mpenzi wako, na unaogopa kwamba anaweza kukuumiza wewe au watoto wako, unaweza kwenda kwenye Mahakama ya Familia na uombe “amri ya kuzuia” (iliyofafanuliwa kwa undani zaidi hapa chini katika sehemu inayohusu “Sheria ya familia na HIV”). Mahakama inaweza kumuamuru mpenzi wako kukaa mbali na wewe na watoto wako, au kumuamuru mpenzi wako kutowasiliana na wewe kwa njia yoyote ile.

Uwezekano mwingine ni kwenda kwenye mahakama ya jinai ili kumwomba Jaji wa Amani “dhamana ya amani” ambayo ni amri ya mahakama ambayo humwambia mtu “kudumisha amani” na awe na tabia nzuri. Kama vile amri ya kuzuia, dhamana ya amani inaweza kumuamuru mtu kukaa mbali na wewe, familia yako, nyumba yako, na maeneo unayoenda, na hata pia kumuamuru mtu huyo kutowasiliana na wewe. Mahakama inaweza pia kupendekeza kwamba wahusika wote wawili watie saini dhamana ya amani ya “pamoja”, ambayo ina maana

kwamba wewe na mtu huyo mwingine mnatoa ahadi ya “kudumisha amani.” Kutia saini dhamana ya amani hakusababishi rekodi ya jinai, lakini kukiuka mahitaji ya dhamana ya amani ni kosa la jinai ambalo linaweza kusababisha kifungo. Ni muhimu kupata ushauri wa kisheria kutoka kwa wakili wa jinai kabla ya kutia saini dhamana ya amani.

Ikiwa mpenzi wako anatumia hali yako ya HIV kukudhulumu, unapaswa kueleza mahakama. Ulinzi dhidi ya dhuluma ya aini hii unaweza kuongezwa kwenye amri ya kuzuia au dhamana ya amani. Unaweza pia kufikiria kupata ushauri wa kisheria haraka ili uweze kujua kama kuna jambo unaloweza kufanya ili kulinda faragha yako.

Iwapo mpenzi wako hatafuata sehemu yoyote ya amri ya kuzuia au dhamana ya amani, unaweza kupiga simu kwa polisi, na polisi watamshtaki kwa uhalifu.

Ikiwa una hofu kwamba aliyekunyanyasa atakuumiza, hakuna yoyote kati ya machaguo haya linalokuhakikishia kwamba utakuwa salama. Ni muhimu kuwa na mpango kamili wa usalama tayari, hata kama mahakama imemuamuru aliyekunyanyasa kukaa mbali na wewe. Unaweza kuwasiliana na makazi ya wanawake ya eneo lako au shirika la usaidizi ili upate msaada wa mpango wa usalama.

**Je, unaweza kupata fidia ya kifedha kwa kudhulumiwa?**
Katika Ontario unaweza kuomba fidia (pesa) kutoka kwa Halmashauri ya Kufidia Majeraha ya Uhalifu -Criminal Injuries Compensation Board (CICB) ikiwa uliponea uhalifu au wewe ni (mwathirika) wa uhalifu. CICB ni mpango wa serikali ambao unaweza kupeana pesa kwa watu ambao wamejeruhiwa au wana gharama zinazotokana na uhalifu. Majeraha yanaweza kuwa ya kimwili au ya kisaikolojia. CICB inaweza kulipa jumla ya malipo mara moja au kila mwezi. Pesa hizo zimetoka kwa CICB na zimelipwa na serikali ya Ontario, sio mtu aliyetekeleza majeraha hayo. Wasiliana na HALCO kwa ushauri wa kisheria kabla ya kuwasilisha maombi kwa CICB. Hupaswi kuchelewa kupata ushauri wa kisheria kwa sababu kuna muda uliotengwa wa kuomba CICB.

Mahakama za raia (tofauti na mahakama za jinai) zinaweza pia kupeana fidia kwa majeraha. Mahakama hizi zinaweza kumuamuru mtu huyo aliyesababisha majeraha hayo kukulipa pesa hizo. Majeraha hayo yanaweza kutokana na mgusano usiotaka wa kimwili, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kingono, na yanaweza pia kujumuisha majeraha ya kisaikolojia. Kiasi cha fidia kinahusiana na uzito wa majeraha na athari kwa maisha yako. Unapaswa kuwasiliana na wakili wa majeraha ya kibinafsi kabla ya kuanza maombi ya CICB au mashtaka. Hupaswi kuchelewa kupata ushauri wa kisheria kwa sababu kuna muda uliotengwa wa kuomba mahakama. Kwa maelezo zaidi kuhusu kupata wakili, angalia nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu.

## Sheria ya Familia na HIV

Sheria ya familia husimamia masuala ya aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

- kutengana na talaka;
- malezi, kuwafikia watoto, na msaada kwa watoto;
- msaada kwa mwanandoa; na
- ugawanyaji wa mali ya familia na nyumba ya familia.

Sheria ya familia husimamiwa na sheria za kitaifa na za mkoa. Mahakama zinaweza kutoa amri kuhusu masuala ya kisheria ya familia. Sheria ya familia inaweza kuwa tata, kwa hivyo

unapaswa kutafuta ushauri wa kisheria kutoka kwa wakili wa sheria ya familia kuhusu haki na machaguo yako.

Kuna kanuni ambazo zinaathiri iwapo na jinsi ambavyo amri za mahakama ya familia ya mkoa zinatekelezwa kwa jamii Asili za Taifa (kwenye hifadhi). Ikiwa unaishi kwenye hifadhi, wasiliana na wakili wa sheria ya familia kwa ushauri wa kisheria. Katika masuala yote ya sheria ya familia, hali yako ya kuwa na HIV pekee haipaswi kamwe kuamua kama:

- utapewa malezi au utaweza kumfikia mtoto wako;
- unafaa kupokea msaada kwa watoto na mwanandoa; au
- utapewa mgao sahihi wa mali ya familia.

Hali yako ya kuwa na HIV haipaswi kuwa muhimu katika sheria ya familia isipokuwa kama inaathiri jinsi unavyomlea mtoto wako au kujitunza mwenyewe.

Iwapo umepitia ukatili kutoka kwa mpenzi wako wa karibu, kuna mpango wa wahudumu wa mahakama ya familia ambao unaweza kukusaidia katika mchakato wa mahakama ya familia. Kwa maelezo zaidi kuhusu mpango huu, angalia sehemu ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu.

**Je, ni machaguo gani ambayo sheria ya familia hutoa ili kuwalinda watu waliopitia dhuluma?**

Mahakama ya sheria ya familia inaweza kumuamuru mpenzi wako kufanya au kutofanya mambo fulani. Unaweza kupata amri ya kumzuia mpenzi wako kukufikia ikiwa mnaishi au mlikuwa mkiishi pamoja, na unaogopa eti atakuumiza wewe au mtoto wako. Amri za kumzuia zinaweza kumuamuru:

- asiwasiliane na wewe na/au (wa) mtoto kwa njia yoyote ile — kwa mfano, kwa kukupigia simu, kukutumia ujumbe, barua pepe, Facebook au kupitia mtu mwingine;
- akae mbali na nyumba yako, kazini kwako, shule ya mtoto wako au maeneo mengine unayopendelea kwenda mara kwa mara; na
- akae katika umbali fulani kutoka kwako na/au mtoto wako.

Amri za malezi na kuwafikia watoto huelezea ni nani ana haki ya kisheria ya kufanya maamuzi yote muhimu kumhusu mtoto (malezi) na ni nani anaweza kuwa na haki ya kisheria ya kumtembelea mtoto (kumfikia). Katika hali za ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu, mahakama inaweza kuamuru muda na maeneo fulani maalum ambapo mzazi wa kumtembelea mtoto anaweza kumtembelea mtoto, ikiwa ni pamoja na "ufikiaji unaosimamiwa," unaomaanisha kwamba mtu mwingine lazima awe na mtoto wakati anamtembelea. Katika hali finyu ambapo mahakama inadhani kwamba mtoto hawezi kuwa salama na mzazi, mahakama inaweza kuamuru watoto kutotembelewa.
Ikiwa umeolewa/ulikuwa umeolewa na mpenzi wako, unaweza kuomba amri ya kipekee ya umiliki ambayo inaweza:

- kukuruhusu uishi katika nyumba ya familia bila mwanandoa wako (pamoja na au bila mtoto yeyote);
- kukuruhusu kudumisha umiliki wa rasilimali za familia; na
- kumwagiza mpenzi wako kutokuja kwenye nyumba hiyo.

Amri ya umiliki wa kipekee wa nyumba ya familia haiathiri ni nani anayemiliki nyumba hiyo au kubadilisha haki ambayo wanandoa wote wawili wanayo ya kushiriki thamani ya nyumba ya familia. Kwa kawaida huwa ya muda mfupi hadi kuwe na uamuzi wa mwisho kuhusu umiliki na jinsi ya kugawanya mali ya familia kati ya wanandoa wote wawili.

Unaweza kuwasilisha maombi kwa mahakama ili upate amri za uzuiaji, malezi/kuwafikia watoto, au umiliki wa kipekee kwa misingi ya hali ya haraka au ya dharura. Maombi hayo yanaweza kushughulikiwa kwa haraka, lakini wakati mwingine sio upesi.

**Amri za mahakama hazizuii unyanyasaji au ukatili kila wakati. Huenda aliyekunyanyasa asitii amri ya mahakama.**
Hata hivyo, ni muhimu kufuata amri ya mahakama, na ikiwa amri ya mahakama haijafuatwa, kunaweza kuwa na matokeo mabaya.

Ikiwa unahofia afya yako au ya mtoto wako ya kimwili au ya kiakili au usalama, unapaswa kufikiria kwenda mahali salama kama makao ya wanawake. Unapaswa kuongea na wakili wa sheria ya familia kwa ushauri wa kisheria kuhusu kuomba amri ya uzuiaji, amri ya malezi/kuwatembelea watoto au amri ya umiliki wa kipekee kutoka kwa korti ya familia. Kuna nyenzo zilizoorodheshwa mwishoni mwa mwongozo huu.

**Iwapo mpenzi wako wa zamani ameshtakiwa kwa uhalifu, je, bado unastahili kupata msaada kwa watoto au msaada kwa mwanandoa?**
Wazazi wana jukumu la kuwasaidia watoto wao. Haijalishi kama umeolewa au ulikuwa umeolewa na mzazi yule mwingine wa mtoto wako, au kama mmewahi kuishi pamoja. Mkitengana na mzazi yule mwingine na ujipate unamlea mtoto huyo karibu kila wakati, unaweza kuomba mahakama ya familia amri ya msaada kwa watoto, au amri inayohitaji mzazi mwingine kutoa maelezo kila mara kuhusu mapato yake au juhudi zake za kutafuta kazi iwapo kwa sasa hawezi kufanya kazi. Mzazi wa mtoto wako atahitajika kulipa usaidizi kwa mtoto ikiwa ana zaidi ya mapato ya chini, na hata kama ameshtakiwa kwa uhalifu. Ijapokuwa kuwa gerezani hakumaanishi kwamba mtu atakoma kulipa msaada kwa watoto, mzazi anaweza kujaribu kupinga amri ya msaada kwa watoto ikiwa kuna mabadiliko katika hali, kama vile mabadiliko katika mapato yake.

Ili kubainisha kiasi cha msaada kwa watoto, mahakama itatekeleza maelekezo ya Msaada kwa Watoto. Maelekezo haya yameorodhesha kiasi kilichowekwa cha msaada kwa kila mtoto kulingana na mapapto ya anayelipa msaada na idadi ya watoto katika familia. Kiasi hiki kinaitwa “kiasi cha wastani.” Kwa kawaida, mzazi ambaye mtoto anaishi na yeye kwa wakati mwingi hupokea msaada kwa watoto kutoka kwa mzazi yule mwingine. Unaweza kupata kiungo cha kiasi hicho cha wastani cha msaada kwa watoto katika sehemu ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu.

Wakati mwingine wapenzi wakitengana, mtu mwenye mapato ya juu zaidi hulipa msaada kwa mwanandoa kwa mtu yule mwingine. Ikiwa ulikuwa umeolewa, sheria ziko katika *Sheria ya Talaka*, ambayo inatumika Canada nzima.  Katika Ontario, ikiwa hukuwa umeolewa, unaweza kupata msaada kwa mwanandoa ikiwa ulikuwa ukiishi na mpenzi wako katika uhusiano kwa angalau miaka mitatu (inaitwa wanandoa wa kisheria), au iwapo mliishi pamoja katika uhusiano thabiti kwa kipindi chochote cha muda na mna mtoto pamoja. Kiasi cha msaada kwa mwanandoa kinaweza kuathiriwa iwapo mtu huyo analipia pia msaada kwa watoto. Msaada kwa watoto utachukua kipaumbele ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya watoto yameshughulikiwa.

Majaji lazima wazingatie masuala kadhaa wakati wanaamua kama mpenzi anapaswa kupata msaada baada ya kutengana. Msaada kwa mwanandoa haukusudiwi kuwafidia watu kwa makosa ya wapenzi wao wakati wa uhusiano, kama vile ukatili au aina nyingine za dhuluma, bali unaweza kushughulikia athari zinazoendelea za kifedha za ukatili au dhuluma hiyo.

Ofisi ya Majukumu ya Familia huhakikisha kwamba malipo ya msaada kwa watoto na mwanandoa yanafanywa ili usilazimike kuwasiliana na mpenzi wako wa zamani au kuwafichulia maelezo yako ya mawasiliano.

Sheria tata zinatumika kwa msaada kwa watoto na kwa msaada kwa mwanandoa. Unapaswa kuwasiliana na wakili wa sheria ya familia ili akusaidie kuelewa sheria hizi na mambo mengine ambayo yanaweza kutumika katika hali yako. Unaweza kwenda kwenye Kituo cha Maelezo ya Sheria ya Familia au upige simu kwa Msaada wa Kisheria wa Ontario ili upate maelezo ya kawaida kuhusu msaada kwa watoto na mwanandoa na jinsi ya kuomba msaada huu mahakamani. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu huduma hizi mtandaoni na viungo vya huduma hizi vimeorodheshwa mwishoni mwa mwongozo huu.

**Je, unahitajika kufichua hali yako au ya mtoto wako ya kuwa na HIV iwapo shirika la kuwalinda watoto linahusika na mtoto wako?**

Kufichua hali yako au ya mtoto wako ya kuwa na HIV ni uamuzi wa mtu binafsi. Ikiwa shirika la kuwalinda watoto lina hoja zinazohusiana na HIV, linaweza kuomba maelezo zaidi kuhusu hali yako ya afya iwapo wanaweza kuonyesha kwamba ni jambo la maana. Huenda kukawa na njia za kujitetea kuwa si jambo la maana.

Ikiwa shirika la kuwalinda watoto linajua hali yako ya kuwa na HIV, shirika hilo linahitajika kuiweka siri na kuitumia tu kwa malengo ya kisheria. Wahudumu wa kuwalinda watoto wamefunzwa kufanya kazi na wanawake wanaopitia dhuluma katika mahusiano yao. Huenda umeshuhudia mambo mabaya hapo awali na shirika la kuwalinda watoto. Huenda ulihisi kwamba shirika hilo lilikubagua kwa sababu ya hali yako ya HIV au sababu nyingine. Iwapo mhudumu wa shirika hakusaidii, unaweza kuomba kuongea na msimamizi. Ikiwa hiyo haitatui tatizo hilo, ongea na wakili wa sheria ya familia au HALCO kwa ushauri wa kisheria. Kuna maelezo mwishoni mwa mwongozo huu kuhusu pahali pa kupata msaada wa kisheria.

**Je, mtoto wako anaweza kuchukuliwa kutoka kwako kwa sababu una HIV?**

Mpenzi wako anaweza kukutisha kwamba atafichua hali yako ya kuwa na HIV iwapo utaripoti tabia zake za kukudhulumu au iwapo utaondoka na mtoto wako. Lakini mtoto wako hawezi kuchukuliwa kutoka kwako kwa sababu una HIV. Hakuna chochote kuhusu kuwa na HIV, ambacho kivyake, kinahalalisha kumchukua mtoto wako, kwa sababu karibu mwingiliano wote wa familia na majukumu ya uzazi hayana hatari yoyote ya kweli ya kuambukiza mtu yeyote HIV.

**Je, hali yako ya kuwa na HIV itaathiri maamuzi kuhusu malezi, makazi, au kumfikia mtoto wako?**

Hali yako ya HIV kivyake haipaswi kuathiri maamuzi kuhusu malezi, makazi au kumfikia mtoto wako. Haki na majukumu yako kama mzazi hayabadiliki kwa sababu una HIV.

Mkitengana na mzazi yule mwingine wa mtoto wako, mtalazimika kuamua ni nani anayeweza kumlea mtoto. Malezi yana maana kwamba una haki ya kisheria ya kufanya maamuzi muhimu kuhusu kumlea mtoto wako. Wazazi wote wana haki ya kulea, hata kama wametengana. Iwapo hamuwezi kukubaliana kuhusu jinsi mtoto wenu anapaswa kulelewa na kutunzwa baada ya kutengana, au huhisi salama kuongea na mpenzi wako kuihusu, basi unaweza kuomba mahakama kuamua ni nani atakayekabidhiwa malezi. Mahakama inaweza kuamuru kwamba

mzazi mmoja au wote wawili wawe na haki ya kulea, na pia inaweza kutoa amri kuhusu ni wapi mtoto ataishi. Mahakama inaweza pia kutoa amri kuhusu ufikiaji ambao kila mzazi anaruhusiwa kuwa nao kwa mtoto. Ufikiaji una maana kwamba mzazi ana haki ya kushinda na mtoto na kujua kuhusu maisha ya mtoto, lakini hana haki ya kufanya maamuzi muhimu kuhusu maisha ya mtoto. Mahakama itaamua malezi na ufikiaji wa watoto kulingana na "maslahi ya mtoto" ambayo ni jaribio la kisheria.

Ili kuamua kuhusu malezi, lazima mahakama izingatie kama mzazi amewahi kumdhulumu mpenzi wake, mzazi wa mtoto, mtu yeyote anayeishi katika nyumba yake, au kwa mtoto yeyote. Hii itakuwa sehemu ya uamuzi wa mahakama kuhusu kama mtu anayenyanyasa ana uwezo wa kutenda kama mzazi.

Mambo mengine ambayo mahakama inaweza kuzingatia ili kubainisha maslahi ya mtoto ni:

- ujuzi wa uzazi ambao kila mzazi anao;
- mpango ambao kila mzazi anao wa kulea na kumtunza mtoto;
- uwezo wa kila mtu wa kumkimu mtoto;
- muda ambao mtoto amekuwa katika nyumba, shule, na jamii moja; na
- matakwa na hisia za mtoto.

Ijapokuwa hali yako ya kuwa na HIV kivyake haipaswi kuathiri uamuzi wa mahakama kuhusu malezi, makazi au kumfikia mtoto, masuala yanayohusiana na hali yako ya kuwa na HIV au hali ya mtoto wako ya kuwa na HIV yanaweza kuzingatiwa. Kwa mfano, ikiwa una ugonjwa au upungufu wowote ambao unaathiri uwezo wako wa kumlea mtoto wako, mahakama inapaswa kuzingatia kama uwezo wako wa kutimiza mahitaji ya mtoto umeathirika. Iwapo uwezo wako umeathirika, basi mahakama inapaswa kuzingatia kama unaweza kupata misaada ya kutimiza mahitaji ya mtoto wako, na maslahi ya mtoto wako ni gani.

Bado HIV ina unyanyapaa mwingi na, katika mizozo mikali, mpenzi wako wa zamani anaweza kujaribu kutumia suala hilo dhidi yako. Ongea na wakili wako na wahudumu wako wa msaada kwa ushauri iwapo una hofu kwamba huenda mpenzi wako wa zamani akajaribu kutumia hali yako ya HIV dhidi yako ili kudhalilisha haki zako kama mzazi.

## Sheria ya Uhamiaji na HIV

**Iwapo umepatikana kuwa na HIV wakati wa uchunguzi wa matibabu wa uhamiaji, je, ni nani atakayejua?**
Vipimo vinavyoonyesha kuwa una HIV kutoka kwa uchunguzi wa matibabu wa uhamiaji hushirikiwa na:

- Uraia na Uhamiaji Canada (CIC);
- Mpenzi/mwanandoa wako iwapo amekufadhili. Ikiwa umefadhiliwa na mpenzi/mwanandoa wako, CIC itafichua matokeo yako ya kupatikana na HIV kwa mpenzi/mwanandoa wako siku 60 baada ya CIC kukuelezea kwamba inapanga kufanya hivyo, isipokuwa ubatilishe maombi yako; na
- Mamlaka za afya ya umma nchini Canada. Ikiwa maombi ya kuhamia Canada yameidhinishwa, CIC itafahamisha shirika la afya ya umma la mkoa/himaya utakapokuwa ukiishi (au unakoishi, ikiwa tayari uko Canada) kuhusu hali yako ya kuwa na HIV.

**Je, hali yangu ya uhamiaji itaathirika iwapo nitamwacha mpenzi wangu au kuripoti dhuluma zake kwa polisi?**
Ikiwa wewe ni mkazi wa kudumu, huwezi kupoteza hali hiyo au kufukuzwa Canada kwa sababu umeondoka kwenye uhusiano wenye dhuluma au kuripoti dhuluma. Wakati mwingine mpenzi anayekudhulumu anaweza kukutisha kwamba anaweza kufanya mpenzi au mwanandoa aliyefadhiliwa afukuzwe nchini Canada, ambayo huitwa kufukuzwa nchini, kama sehemu ya udhibiti wake wa udhalimu. Iwapo una wasiwasi kwamba mpenzi au mwanandoa wako atajaribu kufanya ufukuzwe nchini, unapaswa kuongea na wakili wa uhamiaji kuhusu hali na machaguo yako.

Huenda ukapewa hali ya makazi ya kudumu “inayotegemea hali” iwapo uliwasilisha maombi ya kuja Canada kama mwanandoa au mpenzi kabla ya tarehe ya 25 Oktoba 2012, na ulikuwa katika uhusiano wa miaka miwili au chini yake na mfadhili wako, au haukua na watoto pamoja na mfadhili wako wakati wa maombi hayo ya ufadhili. Iwapo una hali ya makazi ya kudumu inayotegemea hali, unatarajiwa kuishi na mfadhili wako kwa miaka miwili ya kwanza baada ya kuwasili kama mwanandoa aliyefadhiliwa, au baada ya kupata hali yako ya makazi ya kudumu inayotegemea hali ikiwa tayari uko Canada. Iwapo utatengana na mfadhili wako kabla ya wakati huo, unaweza kupoteza hali yako ya makazi ya kudumu na huenda usiruhusiwe kuishi nchini Canada. Msamaha unaweza kutekelezwa katika kutengana kulikosababishwa na kudhulumiwa au kutelekezwa na mfadhili (au mwanafamilia wa familia yake) kunakolenga mpenzi/mwanandoa aliyefadhiliwa, mtoto wake, au mwanafamilia ambaye kwa kawaida huishi katika nyumba yake. Ikiwa uko katika hali hii, ni muhimu kuongea na wakili wa uhamiaji haraka.

Ikiwa uko katikati ya mchakato wa maombi ya kufadhiliwa kama “Mwanandoa au Mpenzi wa Kisheria nchini Canada” na uondoke katika uhusiano huo, au unafikiria kuondoka, unapaswa kupata ushauri wa kisheria haraka. Iwapo mpenzi au mwanandoa ataondoa ufadhili au mtengane wakati maombi yanachakatwa, hutastahiki kupata hali ya makazi ya kudumu kama Mwanandoa au Mpenzi wa Kisheria na huenda ukalazimishwa kuondoka Canada. Huenda bado ukastahili kufuatilia maombi ya kusalia nchini Canada kwa misingi ya hisani na huruma.

Watu wengi wako nchini Canada kihalali bila hali ya kudumu (wana hali ya muda tu). Kwa mfano, wanaweza kuwa na vibali vya kufanya kazi au kusoma, au huenda waliruhusiwa kuingia Canada kama wageni kwa kipindi fulani cha muda. Baada ya hali halali kuisha, watu hawa huwa wako nchini Canada bila hali halali ya uhamiaji. Ikiwa uko nchini Canada bila hali halali ya uhamiaji, maafisa wa uhamiaji wanaweza kukupata na kukufukuza nchini. Ukijaribu kumwacha anayekunyanyasa au uripoti dhuluma hiyo, huenda anayekunyanyasa akakutisha kwamba atakuripoti kwa mamlaka ya uhamiaji. Ni muhimu sana kwamba uongee na wakili wa uhamiaji haraka iwapo unafikiria unaweza kumwacha mpenzi wako au kuripoti dhuluma zake. Wasiliana na HALCO kwa maelezo zaidi haraka iwezekanavyo.

**Je, kuhukumiwa kwa sababu ya uhalifu kuna matokeo gani kwa hali yangu ya uhamiaji?**
Ikiwa wewe si raia wa Canada, kuna hatari ya kuambiwa uondoke (kufukuzwa) Canada iwapo utahukumiwa kwa uhalifu. Iwapo polisi wamewasiliana na wewe au ikiwa una wasiwasi kwamba unaweza kushtakiwa kwa kutekeleza uhalifu na wewe si raia wa Canada, unapaswa kuwasiliana na wakili wako wa uhamiaji haraka, hata kama una makazi ya kudumu na/au ulikuja Canada kama mkimbizi. Unapaswa pia kuwasiliana na wakili wa jinai haraka na umweleze wakili huyo wa jinai kuhusu hali yako ya uhamiaji.

## Sheria ya jinai na HIV

> *Lengo la sehemu hii ni sheria ya jinai, ngono na HIV. Haishughulikii masuala yote ya kisheria kuhusu HIV na ufichuzi. Kwa mfano, kuna uwezekano kwamba kuna jukumu la kisheria la kufichua hali yako wakati unashiriki sindano ili kuingiza dawa mwilini, na inawezekana pia kwamba unaweza kushtakiwa katika mahakama ya raia na mpenzi wako kwa kutofichua hali yako ya HIV kabla ya kufanya mapenzi. Unaweza kuwasiliana na HALCO kwa maelezo kuhusu masuala mengine ya kisheria, ikiwa ni pamoja na masuala mengine ya kufichua hali ya HIV.*

Kufichua hali yako ya kuwa na HIV humaanisha kumweleza mtu mwingine kwamba una HIV. Katika hali nyingi, kuamua kufichua ni chaguo lako. Huna wajibu wowote wa kuwaeleza watoto wako, wanafamilia wengine au marafiki kwamba una HIV.

**Lakini, kufichua hali ya HIV kwa wapenzi unaofanya nao ngono ni tofauti kabisa.**

**Je, sheria ya jinai inasema nini kuhusu ngono na HIV?**
Hakuna sheria ambayo inashughulikia hasa ufichuzi wa hali ya HIV katika *Sheria ya Jinai.* Lakini katika mwaka wa 2012, Mahakama Kuu ya Canada iliamua kwamba ukiwa na HIV, una jukumu la kisheria la kufichua hali yako ya HIV kabla ya kitendo chochote cha ngono ikiwa kuna “uwezekano wa kweli” kwamba utamwambukiza mpenzi wako HIV wakati wa kitendo hicho cha ngono. Ukikosa kumweleza mpenzi wako unayefanya naye tendo la ngono kwamba una HIV kabla ya tendo hilo la ngono, unaweza kushtakiwa kwa kosa kubwa la jinai, *hata kama hujamwambukiza HIV.* Mahakama yanachukulia kutofichua hali ya HIV kuwa uhalifu wakati:

- kitendo hicho cha ngono kati yako na mtu mwingine kinasababisha “uwezekano wa kweli wa kuambukiza HIV”;
- hukufichua hali yako ya kuwa na HIV kabla ya kushiriki ngono; na
- mtu uliyefanya naye tendo hilo la ngono hangekubali kufanya mapenzi iwapo angelijua hali yako ya HIV.

**Je, ni lini una jukumu la kisheria la kufichua hali yako ya kuwa na HIV kabla ya tendo la ngono?**
Jukumu la kisheria la kufichua hali yako ya kuwa na HIV kwa mpenzi unayeshiriki ngono naye linahusiana na kiwango cha hatari ya kuambukiza HIV. Mahakama huamua ni vitendo vipi vya ngono na hali ambazo zinasababisha “uwezekano wa kweli wa maambukizi.” Katika hali nyingine, huenda usiwe na jukumu la kufichua hali yako (angalia hapa chini).

Kufichua hali yako ya HIV ni uamuzi wa kibinafsi sana iwe una jukumu la kisheria au la. Unaweza kupiga simu kwa HALCO ili upate ushauri wa kisheria kabla ya kuamua kufichua hali yako.

Ijapokuwa sheria inaweza kubadilika au kutumika vitofauti katika kesi fulani, chini ya sheria ya sasa kuna jukumu la kisheria la kufichua maambukizi yako ya HIV kabla ya:

- kitendo cha ngono ya uke au ya mkundu bila kondomu; na

- kitendo cha ngono ya uke au mkundu kwa kutumia kondomu *isipokuwa* kama una kiwango cha chini cha virusi vya ukimwi (angalia hapa chini kwa maelezo zaidi kuhusu kiwango cha virusi vya ukimwi).

Mahakama hazijaamua jinsi sheria ya jinai inavyotumika kwa ngono ya mdomo, iwe kupeana au kupokea ngono ya mdomo.

Jukumu la kisheria la kufichua maambukizi yako ya HIV linatumika kwa wapenzi wako *wote* unaofanya ngono nao, iwe umeolewa, mnaishi pamoja, mnachumbiana, au mnashiriki katika ngono na unalipwa, au kufanya ngono kiholela.

Kudanganyana kuhusu hali yako ya HIV ni sawa, au mbaya zaidi, kuliko kutofichua hali yako ya HIV. Unaweza kushtakiwa *hata kama:*

- hukukusudia kumdhuru mpenzi wako; au
- mpenzi wako hakuambukizwa HIV kwa kitendo cha ngono na wewe.

**Je, ni lazima ufichue hali yako ikiwa mpenzi wako unayeshiriki naye ngono pia anaishi na HIV?**
Kuna hatari kwamba unaweza kushtakiwa na kufungwa kwa kutomwambia mpenzi wako mwenye HIV kwamba una HIV. Hata hivyo, hali hizi ni nadra sana na kulingana na ufahamu wetu, hazijahusisha hali ambazo mpenzi wa kingono wa anayetuhumiwa alifichua hali yake ya HIV kabla ya kitendo cha ngono kufanyika. Tafadhali wasiliana na HALCO kwa maelezo zaidi kuhusu suala hili.

> ***"Kiwango cha virusi vya ukimwi"*** *ni kiwango cha HIV katika mwili wa mtu. Kiwango cha virusi vya ukimwi hupimwa kwa kipimo cha damu.*
>
> ***"Isiyoweza kuonekana"*** *humaanisha kwamba kiwango cha HIV katika damu kiko chini sana hadi hakiwezi kuonekana kwa kipimo cha damu cha kiwango cha virusi vya ukimwi. Hata kama una kiwango cha virusi vya ukimwi ambacho hakiwezi kuonekana, bado una HIV. Lengo la matibabu ya kupunguza makali ya HIV (ARV) ni kupunguza kiwango hicho cha virusi vya ukimwi hadi kiwe kisichoweza kuonekana.*
>
> ***"Kiwango cha chini cha virusi vya ukimwi"*** *humaanisha kwamba kiwango cha HIV katika damu kinaweza kugunduliwa katika kipimo lakini kiko chini sana katika mizani. Katika mwaka wa 2012, Mahakama Kuu ya Canada haikubainisha kiwango cha "chini" cha virusi vya ukimwi kinapaswa kuwa kipi wakati wa kuamua iwapo kuna jukumu la kufichua maambukizi yako ya HIV. Kulingana na maamuzi ya Mahakama, angalau kiwango chochote cha virusi vya ukimwi kilicho chini ya rudufu 1,500 kwa mililita kinapaswa kuzingatiwa kuwa cha "chini" lakini bado hatuna uhakika kiwango cha mkato kinapaswa kuwa kipi.*

**Je, ni lini ambapo huna jukumu la kisheria la kufichua hali yako ya HIV kabla ya tendo la ngono?**
Mahakama zinaweza kuamua vitofauti kulingana na ushahidi wa kila kesi, lakini kwa wakati huu, *hakuna* jukumu la kisheria la kufichua hali yako kwa mpenzi unayeshiriki naye ngono:

- wakati kondomu imetumiwa vizuri na haijapasuka na mtu anayeishi na HIV ana kiwango cha chini au kisichoonekana cha virusi vya ukimwi;
- wakati vitendo vya ngono bila hatari — au kiwango cha chini sana cha hatari — ya maambuki ya HIV vinahusika (kwa mfano, kubusu, kupigana punyeto, ngono ya mdomo kwa kutumia kondomu).

**Si dhahiri ni nini kinachoweza kufanyika iwapo kondomu itapasuka wakati wa kitendo cha ngono ambapo mtu mwenye HIV ana kiwango cha chini cha virusi vya ukimwi. Huenda ukawa na jukumu la kufichua hali yako haraka iwezekanavyo baada ya kondomu kupasuka. Ikiwa mpenzi wako anajua kwamba una HIV, anaweza kuamua ikiwa atatafuta "tiba ya kuzuia maradhi baada ya kuambukizwa" (PEP) kwa kutumia dawa za kuzuia HIV. Unapaswa kuanza kutumia PEP haraka baada ya kuambukizwa, ndani ya saa zisizozidi 72.**

**Lakini fahamu kwamba kufichua hali yako baada ya kondomu kupasuka kunaweza kuongeza hatari ya mpenzi wako unayeshiriki naye ngono kuwasiliana na polisi, ambayo inaweza kusababisha kushtakiwa kwa makosa ya jinai. Au mpenzi wako unayeshiriki naye ngono anaweza kukasirika vibaya, ambayo inaweza kusababisha mgogoro au vita.**

Kumbuka kwamba sheria ya jinai inahusu kutofichua; kutomweleza mpenzi wako unayeshiriki naye ngono kwamba una HIV. Sio kosa la jinai iwapo ulifichua hali yako ya HIV kabla ya tendo la ngono na mpenzi wako akakubali kushiriki ngono na wewe, hata kama hutatumia kondomu na/au kiwango chako cha virusi vya ukimwi kiko juu. Hata hivyo mamlaka za afya ya umma, zinaweza kuhusika hata kama ufichuzi ulifanyika. Kwa maelezo zaidi kuhusu sheria ya afya ya umma, tafadhali angalia sehemu inayohusu "Sheria ya afya ya umma na HIV."

**Itakuwaje kama kufichua hali yako ya kuwa na HIV kunaweza kusababisha ukatili?**
Kwa bahati mbaya, sheria haikubali vizuri ukweli wa dhuluma, ugumu wa kufichua hali ya mtu ya kuwa na HIV, au ukweli kwamba baadhi ya watu wanahisi hawawezi kufichua hali yao kwa sababu wanaogopa kuwa wataumizwa kwa njia moja au nyingine. Ikiwa mwanamke hayuko salama, huenda asiwe na uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu ngono, ikiwa ni pamoja na ni lini anapaswa kushiriki ngono, anapaswa kushiriki ngono na nani, au kama kondomu zitatumika.

Huenda mahakama ikakubali kwamba mtu anayeshi na HIV hahitajiki kufichua hali yake kama ana hofu ya kuumia kama kutokana na ufichuzi huo, au kama analazimishwa kushiriki ngono kupitia ukatili au vitisho. Hata hivyo, hakujakuwa na kesi zilizoripotiwa nchini Canada ambapo mahakama ilishughulikia masuala haya, kwa hivyo bado hakuna jibu wazi.

**Je, ni nini hufanyika ikiwa utashtakiwa kwa kutofichua hali yako ya kuwa na HIV kwa mpenzi unayeshirika naye ngono?**
Ikiwa mtu anayeishi na HIV atamweka mtu mwingine katika hali ya "uwezekano wa kweli" wa maambukizi ya HIV wakati wa kushiriki ngono lakini hakufichua hali yake ya HIV kabla ya kushiriki ngono, polisi wanaweza kuchunguza na kumshtaki mwanamke huyo anayeishi na HIV kwa kosa kubwa la jinai, hasa unyanyasaji mkali wa kingono .

Iwapo polisi wanataka kumuuliza maswali au kumkamata, sio lazima ajibu maswali yao. Lakini, anapaswa kuwaeleza polisi maelezo ya kawaida kama vile jina lake na tarehe ya kuzaliwa. Kitu chochote atakachosema kwa polisi wakati wowote kinaweza kutumika dhidi yake. Ana haki ya

kuongea na wakili kwa faragha. (Kwa maelezo zaidi kuhusu usaidizi wa kisheria na kupata wakili, angalia sehemu ya nyenzo mwishoni mwa mwongozo huu.)

Baada ya kumkamata na kumuuliza maswali mwanamke anayeishi na HIV, polisi wanaweza kumwachilia kutoka kwenye kituo cha polisi au kumweka jela. Anaweza kuomba dhamana ili aweze kuachiliwa kutoka kwa jela hadi kesi yake iwe imeamuliwa. Iwapo mahakama itakataa kumwachilia, atalazimika kubaki jelani kesi yake inapokuwa ikiendelea.

Picha yake, hali yake ya HIV, maelezo mengine ya kibinafsi na uhalifu aliotuhumiwa kuutekeleza unaweza kutokea kwenye taarifa za polisi kwa vyombo vya habari na kwenye intaneti. Kwa kawaida, kesi za mahakama ya jinai hufunguliwa kwa umma na vyombo vya habari.

Anaweza kumwajiri wakili wa kumtetea mahakamani. Kulingana na kipato chake, usaidizi wa kisheria unaweza kumsaidia kulipa wakili wake.

Iwapo atakiri kuwa na makosa, au iwapo mahakama itaamua ana makosa, kwa hakika atatumikia kifungo gerezani. Atakuwa na rekodi ya uhalifu. Kwa hakika jina lake litawekwa kwenye orodha ya kitaifa na mkoa ya wahalifu wa ngono. Kwa hakika sampuli ya DNA itachukuliwa kutoka kwake na kuwekwa kwenye benki ya data ya wahalifu waliohukumiwa kutumikia kifungo.

Iwapo mashtaka hayo yataondolewa au apatikane kuwa “hana hatia”, ataachiliwa huru.

Mtu mwenye rekodi ya uhalifu huenda asiweze kuenda katika baadhi ya nchi. Na huenda asiweze kupata aina fulani za kazi.

Kama yeye si raia wa Canada, mamlaka za uhamiaji zinaweza kumfukuza nchini.

**Iwapo polisi watawasiliana na wewe au mashtaka yafunguliwe dhidi yako, unapaswa kuwasiliana na wakili wa jinai haraka kwa msaada. Ikawa tayari hujafanya hivyo, unapaswa pia kupiga simu kwa HALCO. Ikiwa polisi wametoa, au wanakusudia kutoa maelezo kukuhusu, wasiliana na HALCO haraka. Ikiwa wewe si raia wa Canada, ni muhimu sana kwamba uongee na wakili wa uhamiaji pia. Mashtaka au hukumu za jinai zinaweza kuathiri uwezo wako wa kuishi nchini Canada (angalia sehemu iliyoko hapa juu inayohusu “sheria ya uhamiaji na HIV”).**

> *Ijapokuwa sheria ya jinai kuhusu kutofichua hali ya HIV ni kali na matokeo yake yanaweza kuwa mabaya sana, ni muhimu kuweka hatari ya mashtaka ya jinai na uwezekano wa kuhukumiwa katika muktadha. Mwishoni mwa mwaka wa 2014, takriban watu 75,500 nchini Canada walikuwa wanaishi na HIV. Wakati mwongozo huu uliandikwa mnamo Februari 2016, takriban watu 175 nchini Canada walikuwa wameshtakiwa kwa kutofichua maambukizi yao ya HIV kwa wapenzi wao kabla ya kushiriki ngono. Kati ya hizi, takriban kesi 17 ziliwahusisha wanawake walioshtakiwa kwa kutofichua hali zao za kuwa na HIV kwa wanaume kabla ya kushiriki ngono.*

**Je, unawezaje kupunguza hatari ya mashtaka na hukumu za jinai?**

Katika kesi ya jinai, Mwendesha mashtaka (wakili wa serikali) lazima athibitishe bila shaka kwamba mtu aliyetuhumiwa alitekeleza uhalifu huo. Hii ina maana kwamba ni lazima Mwendesha mashtaka awasilishe ushahidi mbele ya mahakama. Mwendesha mashtaka anaweza pia kutumia kitu chochote unachomweleza mtu mwingine kuhusu historia yako ya vitendo vya ngono kama ushahidi dhidi yako katika kesi ya jinai, kwa hivyo fikiria kwa makini kabla ya kuongea na mtu yeyote kuhusu ufichuzi wako wa HIV na vitendo vya ngono ulivyoshiriki. Ruhusa ya kipekee ni wakili kwa sababu, isipokuwa katika hali nadra sana, kila kitu unachomwelezea wakili ambaye amekubali kusikiliza kesi yako na pengine kukuwakilisha ni cha siri na hakiwezi kutumika dhidi yako mahakamani.

Hakuna njia ya hakika ya kuepuka kushtakiwa kwa kutofichua hali ya HIV. Iwapo utashtakiwa, polisi watachunguza na huenda waamue au wasiamue kukufungulia mashtaka. Hapa kuna baadhi ya mambo ambayo unaweza kufanya *kabla* ya kushiriki ngono ili kujilinda mwenyewe dhidi ya kushtakiwa:

- Waeleze wapenzi wako unaoshiriki nao ngono kwamba unaishi na HIV.
    - Weka ushahidi wa kwamba umewafichulia wapenzi wako, kama vile nakala za barua, barua pepe, ujumbe au ushahidi wa maandishi wa kuonyesha kwamba wanajua.
    - Fichua mbele ya shahidi anayeweza kuaminika, kama vile rafiki, na uhakikishe shahidi ameandika tarehe na kilichosemwa na akutumie maelezo hayo ili uyaweke salama.
    - Shiriki katika miadi ya ushauri ya wapenzi mkiwa pamoja na daktari, muuguzi au mhudumu wako wa jamii katika kliniki au hospitali yako, au na mshauri katika shirika la huduma za UKIMWI (ASO), na kwa uwazi ufichue hali yako ya HIV kwa mpenzi wako katika miadi hiyo, kabla ya kushiriki kitendo chochote cha ngono, ufichuzi ambao unaweza kuandikwa na kuhifadhiwa kwenye faili yako.

- Ukiamua kutofichua hali yako:
    - hakikisha unatumia kondomu ya mpira kila wakati; na
    - umwone daktari wako mara kwa mara ili ujaribu kuhakikisha kiwango chako cha virusi vya ukimwi kiko chini zaidi iwezekanavyo. Muulize daktari wako akupime kiwango chako cha virusi vya ukimiwi mara kwa mara ili uwe na ushahidi kwamba kiwango chako cha virusi vya ukimwi kiko chini au hakiwezi kuonekana.

**Je, ni wapi ninaweza kupata usaidizi kuhusu ufichuzi wa HIV?**
Kuwaeleza wengine kwamba una HIV inaweza kuwa vigumu na inaweza kusababisha wasiwasi. Hujui jinsi mtu anavyoweza kuichukulia. Unaweza kuogopa kukataaliwa, ukatili au kuachwa na mpenzi wako au watu wengine. Unaweza kuwa na wasiwasi kwamba watatumia hali yako ya kuwa na HIV dhidi yako au kwamba watawaeleza wengine kuhusu hali yako. Huenda ukawa hasa na wasiwasi kuhusu faragha yako ikiwa unaishi katika jamii yenye watu wachache ambao wanashiriki utamaduni au lugha yako, au watu wanaojuana sana. Huenda ukaogopa kwamba wanafamilia au wanajamii wengine watakukataa au kukuacha au hata kuwa wakatili wakijua hali yako ya HIV au tabia zako za kushiriki ngono. Wasiwasi huu unaweza kuwa mkubwa zaidi wakati huna pesa au rasilimali za kutosha za kuhama, au kama huna hali halali ya uhamiaji nchini Canada.

Kuwasiliana na ASO ya eneo lako au shirika la afya ya wanawake inaweza kuwa hatua nzuri ya kwanza lakini unapaswa kujua kwamba maelezo unayoshiriki na wengine yanaweza kutumika katika kesi ya mahakama. Rekodi za huduma ya afya za watu walioshtakiwa kwa kutofichua hali

zao za HIV hutumika katika kesi karibu zote au zote za mahakamani. Rekodi kutoka kwa mashirika mengine ya usaidizi zimetumika pia katika kesi za mahakama. Mashirika ambayo yanatoa usaidizi yameorodheshwa mwishoni mwa mwongozo huu.

## Sheria ya afya ya umma na HIV

Nchini Canada, kila mkoa na himaya ina sheria za kulinda afya ya umma. Mamlaka ya afya ya umma zina wajibu wa kisheria wa kulinda afya ya umma. Katika Ontario, afya ya umma imepangwa katika maeneo 36 tofauti, kila moja ikiwa na kitengo chake cha afya ya umma. Vitengo vya afya ya umma vinawajibika kisheria kulinda afya ya umma kwa kujaribu kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na HIV. Kitengo cha afya ya umma katika eneo moja kinaweza kutumia uwezo wake vitofauti ikilinganishwa na kitengo kingine cha afya ya umma katika eneo lingine. Ili kuzuia maambukizi ya HIV, mamlaka ya afya ya umma kwa kawaida yatahitaji ufichue kwamba una HIV kwa kila mpenzi unayeshiriki naye ngono na *pia* utumie kondomu.

**Je, mamlaka ya afya ya umma yatajua kwamba ninaishi na HIV?**
Mamlaka ya afya ya umma hujua jina, tarehe ya kuzaliwa, jinsia na maelezo ya mawasiliano ya watu wengi, lakini sio wote, wanaopatikana kuwa na HIV na baadhi ya magonjwa ya zinaa (STI). Kwa maelezo zaidi kuhusu kupimwa HIV na kama mamlaka ya afya ya umma itafahamishwa kuhusu matokeo yako ya kupatikana na HIV, tafadhali wasiliana na HALCO.

**Je, mamlaka ya afya ya umma itawasiliana na mimi?**
Wakati kitengo cha afya ya umma kinajua kwa mara kwanza kwamba unaishi na HIV, kitakushauri kuhusu afya ya ngono, ngono salama, na kuzuia HIV na STI.

**Je, mamlaka ya afya ya umma itawasiliana na mwanandoa wangu au wapenzi wangu ninaoshiriki ngono nao?**
Ikiwa utapatikana kuwa na HIV au STI yoyote, afya ya umma inahitaji kwamba uwasiliane na wapenzi wako unaoshiriki ngono nao, hata kama kwa sasa hamshriki ngono. Hii inajulikana kama kufuatilia mhusika, ushauri wa wapenzi au arifa kwa wapenzi. Mamlaka ya afya ya umma yanaweza kukuomba maelezo kuhusu wapenzi wako unaoshiriki ngono nao, ikiwa ni pamoja na majina yao. Afya ya umma inahitaji kwamba uwasiliane na wapenzi wako unaoshiriki ngono nao ambao unawajua ili waweze kuambiwa kwamba wako katika hatari ya kupata STI na washauriwe wapate huduma ya matibabu. Mamlaka ya afya ya umma yanaweza kumwarifu mpenzi moja kwa moja au kuhitaji thibitisho kwamba wapenzi wako waliarifiwa. Mamlaka ya afya ya umma hayapaswi kufichua jina lako kwa wapenzi wako, lakini wapenzi wako wanaweza kujua kwamba inakuhusu. Kulingana na hali, mamlaka ya afya ya umma yanaweza kukuruhusu wewe au daktari wako kuwafahamisha wapenzi wako. (Kufuatilia wahusika hutumika pia katika kushiriki sindano.)

**Je, mamlaka ya afya ya umma yanaweza kufanya nini iwapo wanafikiria kwamba ninashiriki ngono ambayo inaweza kuambukiza HIV au STI nyingine?**
Ikiwa una HIV na upatikane kuwa na STI nyingine, mamlaka ya afya ya umma yanaweza kudhania kwamba ulimweka mtu mwingine katika hatari ya kupata HIV. Mamlaka ya afya ya umma yanaweza kukushauri, au kutoa “Amri ya Sehemu ya 22” dhidi yako, au zote. Kwa kuwa sheria ya afya ya umma huzingatia kuzuia wagonjwa wapya wa maambukizi ya HIV, mamlaka yanaweza kutumia uwezo wao wa kisheria kuhitaji ufichuzi wa HIV na ngono salama. Mamlaka ya afya ya umma yana uwezo wa kutekeleza Amri ya Sehemu ya 22 dhidi yako iwapo wana sababu ya kuamini kwamba unashiriki katika ngono ambayo ina hatari ya kuambukiza HIV au STI nyingine, na kama wanaamini amri hiyo inafaa ili kupunguza au kuondoa hatari hiyo.

Kwa kawaida amri hiyo itakueleza kwamba ni lazima

- uhudhurie vikao vya ushauri vinavyotolewa na mamlaka ya afya ya umma;
- uwape mamlaka ya afya ya umma majina ya watu ambao unashiriki ngono nao;
- ufichue hali yako ya maambukizi ya HIV kwa kila mpenzi unayeshiriki ngono na yeye; na
- utumie kondomu kila wakati unaposhiriki ngono.

Iwapo utapewa Amri ya Sehemu ya 22 na unataka kuipinga, una siku 15 tu za kukata rufaa. Unaweza kuwasiliana na HALCO kwa ushauri wa kisheria.

**Je, na ikiwa mimi na mwathirika wa unyanyasaji?**
Amri za afya ya umma zinapaswa tu kushughulikia tabia ambazo unaweza kuzidhibiti. Mamlaka ya afya ya umma yakiwasiliana na wewe kwa sababu wanaamini kwamba unashiriki ngono ambayo ina hatari ya kuambukiza HIV au STI nyingine, lakini hii inahusiana na dhuluma, ongea na wakili haraka iwezekanavyo ili ujadili hali yako na unachoweza kufanya ili kuepuka amri hiyo. Iwapo amri imetolewa, unapaswa kuwasiliana na wakili haraka kwa kuwa kuna siku 15 tu za kukata rufaa. Ikiwa unaishi na HIV, unaweza kuwasiliana na HALCO.

# Nyenzo

## Mashirika ambayo yanatoa ushauri nasaha, msaada na usaidizi katika Ontario

Assaulted Women's Helpline: http://www.awhl.org/
Simu ya saa 24/laini ya simu ya TTY wakati wa matatizo ambayo hailipishwi, isiyotaja jina, ya siri kwa wanawake wanaoishi Ontario ambao wamepitia aina yoyote ya dhuluma (huduma hii inatolewa kwa lugha 150).

- 1 866 863-0511
- 1 866 863-7868 (TTY)

Fem'aide: http://www.femaide.ca/
Simu ya saa 24 /laini ya simu ya TTY ya bila malipo kwa wanawake Wanaozungumza Kifaransa katika Ontario.

- 1 877 336-2433
- 1 866 860-7082 (ATS)

Ontario Government Victim Services Directory: http://services.findhelp.ca/ovss/

- Laini ya simu ya Msaada: 1 888 579-2888

Victim Witness Assistance Program (VWAP): www.ontario.ca/victimservices
Mpango (Unaoendeshwa na Wizara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali) ambao unawasaidia walalamikaji wa ukatili na unyanyasaji wa kimapenzi kutoka kwa wapenzi wa karibu, kupitia kuwaelekeza kwa huduma za ushauri, na hata pia maelezo kuhusu mfumo wa mahakama ya jinai.

- 1 888 579-2888

Kwa orodha ya vituo vya unyanyasaji wa kimapenzi katika Ontario: http://www.draw-the-line.ca/gethelp.html

Kwa orodha ya vituo vya matibabu ya unyanyasaji wa kimapenzi/ukatili wa kinyumbani katika hospitali za Ontario: http://sadvtreatmentcentres.ca/en/view.php?key=42&menu=37&lang=en

Laini ya Simu ya Maelezo ya Afya ya Ngono na UKIMWI katika Ontario

- 1 800 668-2437

The Teresa Group: www.teresagroup.ca
Mipango ya kuwasaidia kina mama wanaoishi na HIV.

- Family Support Coordinator: 416 596-7703 ext. 315

Ontario Aboriginal HIV/AIDS Strategy (OAHAS): www.oahas.org/

HIV 411: https://aso411.ca/
Nyenzo za kupata huduma zinazohusiana na HIV nchini Canada.

**Mashirika ya Eneo Kubwa la Toronto (huenda pia yakawa na maelezo kwa wanawake katika sehemu nyingine za Ontario)**

Women's Health in Women's Hands: http://www.whiwh.com/

- 416 593-7655

METRAC Action on Violence: http://www.metrac.org/

- 1 877 558-5570

Barbara Schlifer Commemorative Clinic: http://schliferclinic.com/

- 416 323-9149
- 416 323-1361 (TTY)

Family Services Toronto: http://www.familyservicetoronto.org/

- Trauma services (pamoja na ukatili wa kimahusiano): 416 595-9618
- David Kelley LGBTQ Counselling Program: 416 595-9618

The 519 Church Street Community Centre: http://www.the519.org/

- The 519 Anti-Violence Program: 416 355-6782

AIDS Committee of Toronto: http://www.actoronto.ca/women

- Women's Support Coordinator:  416 340 8484 ext. 239
- Women's Community Development Coordinator: 416 340-2437 ext. 453 au 276

Africans in Partnership Against AIDS (APAA): www.apaa.ca

- 416 924-5256 au 416 644-1650

Alliance for South Asian AIDS Prevention (ASAAP): www.asaap.ca

- 416 599-2727

Asian Community AIDS Services (ACAS):  http://www.acas.org

- 1 877 630-2227 au 1 877 644-2227

Black CAP: http://black-cap.com/

- 416 977-9955
- Women's Support Coordinator: 416 977-9955 ext. 260

Prisoners with HIV/AIDS Support Action Network (PASAN): www.pasan.org
- 1 866 224-9978
- Women's Community Program Coordinator: 416 920-9567 ext. 225

Toronto People With AIDS Foundation (PWA): www.pwatoronto.org
- 416 506-1400

Family court worker program of the Ministry of the Attorney General:
http://www.attorneygeneral.jus.gov.on.ca/english/ovss/family_court_support_worker_program/
Usaidizi kupitia mchakato wa mahakama ya familia kwa wale ambao wamepitia ukatili kutoka kwa wapenzi wa karibu.
- Laini ya Simu ya Kuwasaidia Waathirika: 1 888 579-2888

## Ushauri wa kisheria

HIV & AIDS Legal Clinic Ontario (HALCO): http://www.halco.org/our-services/legal-services
- 416 340-7790
- Simu ya bila malipo katika Ontario: 1 888 705-8889

Legal Aid Ontario: www.legalaid.on.ca/clinics
Kliniki za kisheria za jamii hutoa huduma za kisheria bila malipo kwa watu katika Ontario.
- 1 800 668-8258
- 1 866 641-8867 (TTY)

The Law Society Referral Service (LSRS): www.lsuc.on.ca/lsrs
Huduma ya mtandaoni ambayo inatoa maelekezo kwa mawakili au wasaidizi wa kisheria kwa hadi dakika 30 za ushauri bila malipo, huduma hiyo inaweza kupatikana kupitia simu ikiwa huwezi kupata kompyuta kwa sababu uko kifungoni, taabani, katika makazi au katika jamii ya mbali isiyokuwa na ufikiaji wa intaneti.
- 1 855 947-5255

## Nyenzo nyingine za kisheria

### Ukatili kutoka kwa mpenzi wa karibu

Community Legal Education Ontario (CLEO) http://www.cleo.on.ca/
Nyenzo za machapisho na mtandaoni za elimu ya kisheria za umma kuhusu mada nyingi za kisheria kwa Kiingereza, Kifaransa na lugha nyingine.
- Agiza nakala zilizochapishwa: 416 408-4420.

*Do you know a woman who is being abused? A Legal Rights Handbook*, CLEO
http://www.cleo.on.ca/en/publications/handbook

*Family violence when a woman is sponsored by a spouse or partner,* CLEO
http://www.cleo.on.ca/en/publications/famvio

Ontario Women's Justice Network (OWJN): www.owjn.org

Maelezo ya kuwasaidia wanusurika wa ukatili na wasaidizi wao kuelewa vyema haki za kisheria katika Ontario.

- 416 392-9138

## Sheria ya familia

Elimu ya Sheria ya Familia kwa Wanawake: www.onefamilylaw.ca
Tovuti hii hutoa nyenzo kuhusu haki za wanawake chini ya sheria ya familia ya Ontario na maeneo mengine ya sheria ambayo ni muhimu wakati familia zinapitia matatizo. Maelezo yanapatikana kwa lugha 14 katika mifumo mbalimbali.

Legal Aid Ontario Family Law Service Centres:
http://www.legalaid.on.ca/en/getting/type_familylawservicecentres.asp

The Ministry of the Attorney General Family Law Information Centres:
http://www.attorneygeneral.jus.gov.on.ca/english/family/infoctr.php

- 1 800 518-7901
- 1 877 425-0575 (TTY)

Kwa maelezo zaidi kuhusu haki za mali katika hifadhi, angalia Mtandao wa Haki za Wanawake Ontario, *Understanding Property Rights on Reserves*
http://owjn.org/owjn_2009/component/content/article/58-aboriginal-law/355-matrimonial-property-rights-reserves

Kwa maelezo zaidi kuhusu Maelekezo ya Kuwasaidia Watoto na kiwango cha wastani cha msaada kwa watoto, angalia Idara ya Haki, *Support Tables*: http://www.justice.gc.ca/eng/fl-df/child-enfant/ft-tf.html.

Resources on family law, CLEO:
http://www.cleo.on.ca/en/resources-and-publications/pubs?language=en&field_legal_topic_tid_i18n=87

*Children's aid: Information for parents*, CLEO
http://www.cleo.on.ca/en/publications/cas-en

## Sheria ya Uhamiaji na HIV

*Criminal charges in Canada and your immigration status*, CLEO
http://www.cleo.on.ca/en/publications/stat-en

*Mothers without Status: Practical information for service providers working with women who have no legal status*, YWCA Vancouver, 2009
http://ywcavan.org/sites/default/files/resources/downloads/YWCA%20Mothers%20Without%20Legal%20Status_2010_web.pdf

*Immigration and Travel to Canada for People Living with HIV: Questions and Answers*, Canadian HIV/AIDS Legal Network, 2015.

http://www.aidslaw.ca/site/canadas-immigration-policy-as-it-affects-people-living-with-hiv-questions-and-answers/

### Sheria ya jinai na HIV

*Women and the Criminalization of HIV Non-Disclosure*, Canadian HIV/AIDS Legal Network, 2013
http://www.aidslaw.ca/site/wp-content/uploads/2013/04/Women_crim-ENG.pdf

*HIV Disclosure to Sexual Partners: Questions and answers for newcomers*, Canadian HIV/AIDS Legal Network
http://www.aidslaw.ca/site/hiv-disclosure-to-sexual-partners-qa-for-newcomers/

*Criminal Law & HIV Non-Disclosure in Canada*, Canadian HIV/AIDS Legal Network
http://www.aidslaw.ca/site/criminal-law-and-hiv/

### Haki za Usiri na HIV

*Know Your Rights: Privacy and Health Records*, Canadian HIV/AIDS Legal Network, 2014
http://www.aidslaw.ca/site/know-your-rights-6-privacy-and-health-records/

*Know Your Rights: Disclosure, Privacy and Parenting*, Canadian HIV/AIDS Legal Network, 2014
http://www.aidslaw.ca/site/know-your-rights-8-disclosure-privacy-and-parenting/

*Privacy and disclosure: questions and answers on HIV-related privacy and disclosure issues for women's service providers*, Canadian HIV/AIDS Legal Network, 2012
http://www.aidslaw.ca/site/privacy-and-disclosure-questions-and-answers-on-hiv-related-privacy-and-disclosure-issues-for-womens-service-providers/

## Shukrani

Mwongozo huu umetengenezwa na Canadian HIV/AIDS Legal Network, the HIV & AIDS Legal Clinic Ontario (HALCO) na METRAC. Ufadhili umetolewa na Law Foundation of Ontario, na Legal Aid Ontario ilitoa huduma za utafsiri wa Kifaransa.

Tunashukuru sana kwa michango ya wahariri wafuatao: Fatimitou Barry, Angela Chaisson (aliyehariri sehemu za "Machaguo ya kisheria kwa wanawake wanaoishi na HIV wanaopita ukatili kutoka kwa wapenzi wao wa karibu"), Marisol Desbiens, Kim Dolan, Karin Galldin, Marlene Ham, Haoua Inoua, Tara Jewel, Julie S. Lalonde, N. Nicole Nussbaum (aliyehariri sehemu inayohusu "Sheria ya familia ya HIV") na wanachama wa Jamii ya Kimataifa ya Wanawake Wanaoishi na HIV (ICW) nchini Canada.